




Hapo zamani za kale,  
kulikuwa na  
mwanamme aliyeitwa  
Biantaka. Alikuwa na  
ng'ombe. Kila siku  
Biantaka alimlisha  
ng'ombe wake na  
kumpa maji. Alikuwa  
na chungu kidogo  
alichotumia kuchota  
maji.



Siku moja, Biantaka alimwendea jirani yake kumuomba chungu kikubwa ili akitumie kuchota maji. Jirani yake alikubali kumwazima Biantaka chungu kikubwa. Alisema, "Tatizo la jirani yangu ni tatizo langu."

Siku chache baadaye, Biantaka alienda kwa mfinyanzi akanunua chungu kidogo. Alipofika nyumbani, alikiweka ndani ya kile chungu kikubwa alichomuomba jirani yake.





Alijitwika chungu kikubwa kilichokuwa na kile  
kidogo ndani yake. Akaenda moja kwa moja  
hadi kwa jirani yake aliyemwazima.



Biantaka alimwambia,  
“Nimekurejeshea  
chungu chako  
ambacho kimezaa  
kingine.” Jirani  
alishangaa kwamba  
chungu chake kilikuwa  
kimezaa chungu  
kingine. Alimpongeza  
Biantaka akisema,  
“Umebarikiwa sana.”



Baada ya muda,  
Biantaka alirudi kwa  
jirani yake kumuomba  
chungu tena. Mara hii,  
kakuwa na nia nzuri.



Mwenye chungu  
alimsubiri Biantaka  
arejeshe chungu  
chake bila mafanikio.  
Mwishowe, alikwenda  
nyumbani kwa  
Biantaka akasema,  
“Nimekuja  
kukichukuwa chungu  
changu.”



Biantaka alimwambia  
jirani yake, "Rafiki  
yangu, chungu chetu  
kilifariki. Nilikusudia  
kuja kukuletea ujumbe  
huo mbaya."



Kwa mshangao, Jirani  
aliruka juu. Uso wake  
ulianza kufura kwa  
hasira. Alipiga kelele  
akimkemea Biantaka,  
“Sijawahi kusikia kuwa  
chungu kinafariki!”



Biantaka alimjibu,  
“Rafiki yangu, lazima  
uyakubali mambo  
haya. Kila kitu  
kinachozaa lazima pia  
kifariki. Mimi pia  
nilihuzunika sana  
kuftuati kifo cha  
chungu chako  
kikubwa.”



Jirani alifoka kwa  
hasira akaenda kortini  
kumshtaki Biantaka.  
Hakimu alisikiliza  
maelezo ya  
pande zote mbili.  
Aliamua kuwa jirani  
mwenye chungu ndiye  
aliyekuwa na makosa.



Hakimu alimwuliza,  
“Biantaka  
alipokwambia kuwa  
chungu chako kilizaa,  
ulikubali. Kwa hivyo  
unapaswa kukubali  
anaposema kwamba  
kila kiumbe hai  
kinachozaa lazima  
kifariki kwa kuwa  
anasema ukweli.”  
Hivyo ndivyo hakimu  
alivyoamua kesi hiyo.



Jirani alitembea polepole kama konokono akarudi nyumbani. Alikuwa amekipoteza chungu chake kikubwa. Naye Biantaka alikuwa amekipata chungu kikubwa kwa kutumia ujanja wake.





